

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Tele: +255 0262322761-5
Fax No. +2550262324218
Email: info@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

Mkutano wa Tisa wa Bunge la Kumi na Moja umeahirishwa hadi Januari 30, 2018 ambapo pamoja na mambo mengine, Bunge limetoa **onyo kali kwa Wahariri wa Magazeti ya Mtanzania, Mwananchi na Nipashe** kwa kosa la kuchapisha na kusambaza mwenendo wa shauri lililokuwa likifanyiwa kazi na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. **Vilevile Bunge limewataka Wahariri wa magazeti hayo kuomba radhi katika kurasa za mbele za magazeti yao ndani ya siku tano kuanzia tarehe ya Leo (17 Novemba, 2017).**

Adhabu hiyo imetolewa Bungeni leo wakati Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai akitoa taarifa fupi kuhusu shauri la kuvunja Haki na Kinga za Bunge linalowahusu Wahariri na Waandishi wa Habari wa Magazeti hayo. Mheshimiwa Spika amemuagiza Mwanasheria Mkuu wa Serikali awafikishe Mahakamani Wahariri hao iwapo watashidwa kutekeleza agizo hilo kama ilivyoamuliwa.

Mnamo tarehe 22 Septemba, 2017, magazeti hayo yalichapisha habari za mwenendo wa shauri na ushahidi uliotolewa na Mhe. Zitto Kabwe (Mb) mbele ya Kamati, kitendo ambacho ni kinyume na kifungu cha 34 (1) (f) na (g) ya Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296.

Kamati ya Maadili ilipendekeza na hatimaye Bunge kuridhia adhabu hiyo kwa wahusika baada ya kuzingatia kuwa Wahariri na Waandishi hao waliitikia wito na kutoa ushirikiano kwa Kamati ikiwemo kukiri na kujutia makosa yao na kwa kuwa ni wakosaji wa mara ya kwanza.

Wahariri na Waandishi wa Habari waliohojiwa na Kamati ya Maadili ni; Ndg. Denis Msacky, Mhariri Mtendaji wa gazeti la Mtanzania, Ndg. Bakari Kimwanga, mwandishi wa habari wa gazeti la Mtanzania, Ndg. Angetile Osiah, Mhariri Mtendaji wa gazeti la Mwananchi, Ndg. Elias Msuya, mwandishi wa habari wa gazeti la Mwananchi, Ndg. Edmond Msangi, Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe na Ndg. Gwamaka Alipipi, mwandishi wa habari wa gazeti la Nipashe.

Kuhusu Mheshimiwa Zitto, Spika wa Bunge aliliambia Bunge kuwa alitakiwa kufika mbele ya Kamati hiyo kwa mara nyingine kwa ajili ya mahojiano kutokana na vitendo vyake ya kuendelea kudharau Bunge hata hivyo bado hajapatikana na pindi akipatikana atatakiwa kufika mbele ya kamati kama alivyohitajika.

Kwa upande mwingine Spika wa Bunge Mheshimiwa Ndugai kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, (Toleo la Januari, 2016,) ameunda Kamati maalum mbili ambazo ni Kamati Maalum ya **Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na sekta ndogo ya gesi** na Kamati Maalum ya **Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na Sekta ya uvuvi**.

Kamati hizo mbili zimeelekezwa kufanya kazi kwa muda wa siku thelathini kuanzia tarehe watakayojulishwa na Katibu wa Bunge na baada ya kukamilisha kazi yake itawasilisha taarifa kwa Spika ili taratibu zingine muhimu zifuata.

Wajumbe walioteuliwa na Spika wa Bunge kuunda Kamati ya **Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na sekta ya uvuvi** ni Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mhe. Tauhida Gallos Nyimbo, Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mhe. Mussa Bakari Mbarouk, Mhe. Cosato David Chumi na **Mhe. Anastazia Wambura ambaye atakuwa Mwenyekiti**.

Kwa upande wa kamati ya **Ushauri kuhusu namna ya kuliwezesha Taifa kunufaika na sekta ndogo ya gesi** walioteuliwa ni Mhe. Innocent Lugha Bashungwa, Mhe. Dustan Luka Kitandula, Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Oscar Rwegasira Mukasa, Mhe. Ruth Hiyob Mollé, Mhe. Richard Philip Mbogo, Mhe. Omar Mohamed Kigua, Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mhe. Sebastian Simon Kapufi na **Mhe. Doto Biteko ambaye atakuwa Mwenyekiti**.

Katika hatua nyingine Spika wa Bunge amewahimiza Waheshimiwa Wabunge kujitokeza kwa wingi katika Mashindano ya Michezo ya Mabunge ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakatofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 1 hadi 11 Disemba 2017.

Mwisho, Spika wa Bunge ameisisitiza Serikali kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya kuutambua Mji wa Dodoma kuwa ni Makao Makuu ya Nchi.

Imetolewa na:- Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano,
Ofisi ya Bunge,
S.L.P 914,
DODOMA.

17 Novemba, 2017